# WIZARA YA KILIMO

# BODI YA KOROSHO TANZANIA

**MWONGOZO WA UPATINAKAJI NA UGAWAJI WA PEMBEJEO BILA MALIPO KWA WAKULIMA NA MABOMBA YA RUZUKU KATIKA ZAO LA KOROSHO MSIMU WA 2022/2023 UNAOTOLEWA CHINI YA SHERIA YA TASNIA YA KOROSHO NA. 18 YA MWAKA 2009 NA KANUNI ZAKE ZA MWAKA 2010**

***Umeandaliwa na:-***

*Bodi ya Korosho Tanzania,*
*S. L. P 533,*
***MTWARA.***

**MEI, 2022**

# YALIYOMO


YALIYOMO .......... ii

TAFSIRI YA MAANA YA BAADHI YA MANENO YALIYOTUMIKA .......... iv

DIBAJI .......... V

1.0 UTANGULIZI .......... 1

2.0 HALI ILIVYO .......... 2

**2.1 Umuhimu wa Tasnia ya Korosho Nchini .......... 2**

**2.2 Utaratibu wa Upatikanaji wa Pembejeo katika Zao la Korosho .......... 2**

**2.3 Matumizi ya pembejeo na uzalishaji wa korosho ghafi .......... 3**

3.0 MADHUMUNI YA MWONGOZO .......... 4

4.0 MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UTAYARISHAJI WA MWONGOZO HUU .......... 4

5.0 UPATIKANAJI WA PEMBEJEO NA MABOMBA KATIKA ZA ZAO LA KOROSHO MSIMU WA MWAKA 2022/2023 .......... 4

6.0 UDHIBITI WA UBORA WA PEMBEJEO NA MABOMBA .......... 6

7.0 MGAO WA PEMBEJEO NA MABOMBA .......... 7

8.0 UTARATIBU WA UGAWAJI WA PEMBEJEO NA MABOMBA KWA WAKULIMA .......... 7

9.0 MUUNDO WA KAMATI YA MAPOKEZI, KAMATI ZA PEMBEJEO WILAYA, KATA NA KIJIJI 9

**9.1 Kamati ya Mapokezi na Usambazaji wa Pembejeo na Mabomba .......... 9**

**9.2 Kamati ya Pembejeo ya Wilaya .......... 9**

**9.3 Kamati ya Pembejeo ya Kata .......... 9**

**9.4 Kamati ya Pembejeo ya Kijiji .......... 10**

**9.5 Kamati ya Pembejeo ya Mkoa .......... 9**

10.0 UTARATIBU WA USAFIRISHAJI WA PEMBEJEO NA MABOMBA KUTOKA GHALA KUU KWENDA KWA WAKULIMA .......... 10

11.0 USIMAMIZI, UFUATILIAJI NA TATHMINI .......... 10

12.0 UTARATIBU WA UGHARAMIAJI KWA WANAOHUSIKA NA USIMAMIZI .......... 10

13.0 MAFUNZO YA MATUMIZI SAHIHI NA SALAMA YA VIUATILIFU NA MABOMBA .......... 11

14.0 UGHARAMIAJI WA PEMBEJEO NA MABOMBA .......... 11

15.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU .......... 11

**15.1 Wizara ya Kilimo .......... 11**

15.2 Sekretarieti za Mikoa ........ 11
15.3 Bodi ya Korosho Tanzania........ 12
15.4 Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)........ 12
15.5 Halmashauri........ 12
15.6 Vyama Vikuu vya Ushirika (Union) ........ 13
15.7 Chama cha Msingi cha Ushirika (AMCOS)........ 13
15.8 TARI Naliendele........ 13
15.9 Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA)........ 14
15.10 Kamati ya Mapokezi na Ugawaji wa Pembejeo ........ 14
15.11 Kamati ya Pembejeo ya Wilaya ........ 14
15.12 Kamati ya Pembejeo ya Mkoa........ 14
15.13 Wazabuni wa Pembejeo na Mabomba........ 14
15.14 Kamati ya Pembejeo ya Kata........ 15
15.15 Kamati ya Pembejeo ya Kijiji ........ 15
15.16 Wakulima wa Korosho........ 15
15.17 Taasisi za Fedha........ 16
15.18 Waandishi wa habari ........ 16
16.0 WAJIBU WA PAMOJA ........ 16
17.0 MUDA WA UTEKELEZAJI ........ 16
18.0 ILANI ........ 16

## TAFSIRI YA MAANA YA BAADHI YA MANENO YALIYOTUMIKA

Katika mwongozo huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| ***"Sheria"*** | maana yake ni Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009; |
| ***"Mwongozo"*** | maana yake ni Mwongozo wa upatikanaji na ugawaji wa pembejeo na mabomba katika zao la korosho nchini kwa msimu wa mwaka 2022/2023 unaotolewa chini ya sheria ya tasnia ya korosho na. 18 ya mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2010; |
| ***"Union"*** | maana yake ni Chama Kikuu cha Ushirika kinachohusika na zao la korosho nchini; |
| ***"MAMCU Ltd"*** | maana yake ni Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya za Mtwara, Masasi na Nanyumbu; |
| ***"TANECU Ltd"*** | maana yake ni Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya za Newala na Tandahimba; |
| ***"TAMCU Ltd"*** | maana yake ni Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya ya Tunduru; |
| ***"RUNALI"*** | maana yake ni Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale; |
| ***"Lindi Mwambao"*** | maana yake ni Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Wilaya za Lindi na Kilwa; |
| ***"CORECU Ltd"*** | maana yake ni Chama Kikuu cha Ushirika kutoka Mkoa wa Pwani; na |
| ***"Wazabuni"*** | maana yake ni makampuni yanayosambaza pembejeo na Mabomba nchini ambayo yamefunga mkataba na Vyama Vikuu vya Ushirika kwa ajili hiyo. |
| ***"TPHPA"*** | *Tanzania Plant Health and Pesticides Authority* (Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania). Zamani ilikuwa ikijulikana kama TPRI *(Tropical Pesticides Research Institute* yaani Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kitropiki). |
| ***"Kamati ya Pamoja"*** | Muungano/Umoja wa Vyama Vikuu vya Ushirika MAMCU Ltd, TANECU Ltd, TAMCU Ltd, CORECU Ltd, RUNALI na LMCU katika ununuzi wa pembejeo, mabomba na magunia kwa ajili ya zao la korosho msimu wa 2022/2023. |

# DIBAJI

Zao la korosho ni mojawapo ya mazao makuu ya biashara nchini yanayoliingizia Taifa letu fedha nyingi ambapo kwa mwaka 2017/2018 zao hilo liliongoza kwa kuingiza fedha za kigeni kiasi cha Dola za Marekani milioni 585.1 sawa na Shilingi za Tanzania trilioni 1.3. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeandaa Mwongozo wa Upatinakaji na Ugawaji wa Pembejeo bila malipo kwa wakulima na mabomba katika zao la korosho msimu wa mwaka 2022/2023. Mwongozo huu umelenga kuboresha utaratibu uliotumika msimu wa 2021/22. Aidha, utekelezaji wa mwongozo huu unatarajiwa kuongeza tija na uzalishaji wa korosho ghafi na hatimaye kuleta manufaa ya kuongezeka kipato kwa wakulima na Taifa kwa ujumla. Tofauti na msimu uliopita, pembejeo za msimu huu zitahusisha mikoa mipya katika kilimo cha korosho. Hivyo, ni matumaini ya Serikali kuwa uamuzi huu utaongeza hamasa kwa wakulima na wadau wote wa korosho katika kufikia lengo la uzalishaji wa korosho ghafi tani 400,000 katika mwaka 2022/2023 na tani 700,000 ifikapo mwaka 2025/2026.

Utayarishaji wa mwongozo huu umeshirikisha makundi yote ya wadau katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho hapa nchini zikiwemo Mamlaka za Serikali ngazi ya Mikoa na Wilaya, Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali. Hivyo, ni matumaini yangu kuwa utekelezaji wa Mwongozo huu utakuwa shirikishi na utaleta manufaa yaliyokusudiwa kwa wadau wote katika tasnia ya korosho hapa nchini.

Natanguliza shukrani zangu kwa ushirikiano wenu.

..........................................

FRANCIS ALFRED

**KAIMU MKURUGENZI MKUU**

**TAREHE** 9 MEI 2022

## 1.0 UTANGULIZI

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali ngazi ya Mikoa na Wilaya, Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zilizopo kwenye mnyororo wa thamani wa zao la korosho hapa nchini, wakulima na wadau wengine wanaendelea na maandalizi ya uzalishaji wa korosho ghafi msimu wa mwaka 2022/2023. Mojawapo ya maandalizi hayo ni upatikanaji wa pembejeo na mabomba ya kupulizia *(Motorized Blowers)* kwa wakulima wote wa korosho nchini.

Katika msimu huu kama ilivyokuwa msimu uliopita Serikali imeelekeza kuwa pembejeo za zao la korosho zilizoagizwa na Vyama Vikuu vya Ushirika, ambazo ni sulphur ya unga tani 25,000 na viuatilifu vya maji lita 1,500,000 zigawiwe kwa wakulima wa korosho bila malipo. Uamuzi huu umelenga kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji wa korosho, na hatimaye kumwongozea kipato. Tofauti na msimu uliopita msimu huu mikoa mipya katika kilimo cha korosho imetengewa asilimia mbili (2%) ya viuatilifu vya maji na mabomba. Mikoa ya asili ambayo ni Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Tanga imetengewa 100% ya sulphur yote na 98% ya viuatilifu vya maji na mabomba. Hivyo, ni matumaini ya Serikali kuwa hatua hii itaongeza hamasa kwa wakulima na wadau wote wa korosho katika kufikia lengo la uzalishaji wa korosho ghafi tani 400,000 katika mwaka 2022/2023 na tani 700,000 ifikapo mwaka 2025/2026.

Aidha, ili kuongeza ufanisi wa mapokezi na usambazaji wa pembejeo za ruzuku na mabomba katika msimu huu Kamati ya Pamoja imeandaa maghala ya kupokelea na kuhifadhi viuatilifu na mabomba yaliyopo eneo la Bandari ya Mtwara chini ya uangalizi wa Meneja Dhamana *(Collateral Manager)* kampuni ya *ACE Global Depository (Tanzania) Limited*. Hivyo wazabuni watatakiwa kuwasilisha shehena ya viuatilifu na mabomba katika ghala hizo ambapo Kamati ya Pamoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika itajiridhisha na kiasi na ubora wa viuatilifu kwa kuchukua sampuli kwa ajili ya vipimo kwenda kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA). Ni muhimu kujiridhisha na ubora *(Quality)* pamoja na kiasi *(Quantity)* cha viuatilifu na mabomba kabla ya kusambazwa kwa wakulima ili kuepuka usumbufu endapo viuatilifu/mabomba vitawafikia wakulima vikiwa na ubora hafifu.

Usafirishaji wa pembejeo na mabomba kutoka maghala yaliyopo Mtwara Mjini kwenda kijijini utafanywa na Vyama Vikuu vya Ushirika chini ya usimamizi wa karibu wa Kamati za Pembejeo ngazi ya Mkoa na Halmashauri husika.

Maandalizi ya Mwongozo huu yemezingatia Sera, Mikakati na Mipango ya Taifa ikiwemo; Dira ya Maendeleo ya Taifa *(Tanzania Development Vision - TDV 2025)*; Mpango wa Taswira ya Muda Mrefu wa Taifa *(Long Term Perspective Plan -LTPP 2012-2021)*; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano *(Third Five Year Development Plan - FYDP III 2021/22-2025/26)*; Sera ya Taifa ya Kilimo ya 2013; Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya 2002; Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(Agricultural Sector Development Program Phase II – ASDP II 2017/18 - 2027/28)*; Mkakati wa Tasnia ya Korosho Nchini 2013/2014 – 2023/2024 *(Cashewnut Industry Strategy 2013/2014 – 2023/2024)* na Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Aidha, Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya 2009 *(The Cashewnut*

*Industry Act No. 18, 2009)*, Sheria ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Na. 4 ya 2020 imezingatiwa. Vilevile, Mwongozo huu umezingatia mipango na program za kikanda na kimataifa zinazohusu sekta ya kilimo ikiwemo Programu Kabambe ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Afrika *(CAADP, 2015-2025)*; Malengo ya Maendeleo Endelevu *(Sustainable Develepment Goals-SDGs)* pamoja na itifaki na mikataba mbalimbali ambayo nchi imeridhia kuhusu matumizi salama ya viuatilifu kwa afya ya wanyama, mimea na mazingira (Mkataba wa Rotterdam na Stockholm).

Pia, Mwongozo huu umezingatia vipaumbele vya Wizara ya Kilimo ambavyo ni Kuongeza tija na kuweka mkazo kwenye utafiti utakaozingatia ugunduzi wa aina za mbegu bora na mbinu bora za kilimo; Kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora; Kuimarisha huduma za ugani; Kuimarisha kilimo cha umwagiliaji; Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo; Kuimarisha kilimo anga kwa ajili ya kudhibiti visumbufu; na Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji.

## 2.0 HALI ILIVYO

### 2.1 Umuhimu wa Tasnia ya Korosho Nchini

Korosho ni mojawapo ya mazao makuu ya biashara nchini yanayoliingizia Taifa letu fedha nyingi za kigeni. Mathalani, msimu wa mwaka 2017/2018 zao la korosho liliongoza kwa kuingiza fedha za kigeni kiasi cha Dola za Marekani milioni 585.1 sawa na Shilingi za Tanzania trilioni 1.3 (Ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania, 2018). Kwa kutambua mchango huu, Serikali imeteua zao la korosho kuwa miongoni mwa mazao ya kimkakati.

Jumla ya Mikoa 20 kutoka Tanzania Bara inalima zao hili ikiongozwa na Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Tanga. Mikoa mingine ni Mbeya, Morogoro, Singida, Dodoma, Katavi, Tabora, Njombe, Rukwa, Kigoma, Shinyanga, Songwe, Iringa, Kilimanjaro, Geita na Manyara. Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo Bodi ya Korosho kuna zaidi ya wakulima wa korosho 318,427 nchi nzima. Hii ni kwa mujibu wa zoezi la usajili wa wakulima wa korosho lililofanyika mwaka 2018/2019.

### 2.2 Utaratibu wa Upatikanaji wa Pembejeo katika Zao la Korosho

Pembejeo za kilimo hususan viuatilifu ni muhimu kwa kuwawezesha wakulima wa zao la korosho kuongeza tija na uzalishaji wa korosho ghafi. Kwa misimu ya nyuma kabla ya msimu wa 2018/2019, Serikali ilitoa ruzuku ya 50% ya pembejeo na mabomba isipokuwa msimu wa 2017/2018 ambapo pembejeo zilitolewa bila malipo kwa wakulima. Kuanzia msimu wa mwaka 2018/2019, pembejeo za zao la korosho nchini zimekuwa zikisambazwa na sekta binafsi (Wafanyabiashara) ambapo wakulima walitakiwa kujigharamia moja kwa moja kwa 100%. Wakulima hao wamekuwa wakinunua pembejeo hizo kwa fedha taslimu au mkopo ambao hata hivyo urejeshaji wake umekuwa siyo wa kuridhisha. Mathalani; msimu wa 2018/2019 hadi msimu wa 2020/2021 Bodi ya

Korosho, Union na Mabenki wamekuwa wahanga wa mikopo waliyotoa kwa wakulima kutorejeshwa kwa wakati.

Utaratibu wa wakulima kujigharamia pembejeo moja kwa moja kwa 100% umeonekana kutoleta matokeo mazuri. Hii ni kutokana na matumizi madogo ya pembejeo kunakosababishwa na wakulima kushindwa kumudu gharama za pembejeo hizo. Mathalani, kumbukumbu zilizopo Bodi ya Korosho Tanzania zinaonesha uzalishaji wa korosho ghafi umepungua kwa tani 103,039 kutoka tani 313,826 msimu wa 2017/2018 hadi tani 210,787 msimu wa 2020/2021.

### 2.3 Matumizi ya pembejeo na uzalishaji wa korosho ghafi


Mwenendo wa tija na uzalishaji wa korosho ghafi hapa nchini kabla na baada ya ruzuku unaonesha kutegemea sana kiasi cha pembejeo kilichotumika na wakulima. Ongezeko la matumizi ya pembejeo kutokana na ruzuku unaonesha kuwa na mahusiano chanya na ongezeko la uzalishaji wa korosho ghafi kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 1**.

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa matumizi ya pembejeo na uzalishaji wa korosho ghafi kuanzia msimu wa 2012/2013 hadi msimu wa 2020/2021.**

| Msimu | Sulphur ya Unga (Tani) | Uzalishaji wa Korosho Ghafi (Tani) |
|---|---|---|
| 2012/2013 | 5,000 | 127,947 |
| 2013/2014 | 5,000 | 129,823 |
| 2014/2015 | 8,000 | 198,114 |
| 2015/2016 | 10,000 | 155,245 |
| 2016/2017 | 15,000 | 265,238 |
| 2017/2018 | 18,000 | 313,826 |
| 2018/2019 | 12,352 | 225,154 |
| 2019/2020 | 8,610 | 232,682 |
| 2020/2021 | 8,731 | 210,787 |
| 2021/2022 | 13,562 | 238,576 |

**Chanzo:** Bodi ya Korosho Tanzania.

**Kielelezo Na. 1: Mwenendo wa matumizi ya pembejeo na uzalishaji wa korosho ghafi kuanzia msimu wa 2012/2013 hadi msimu wa 2020/2021.**




## 3.0 MADHUMUNI YA MWONGOZO

Mwongozo huu pamoja na mambo mengine una dhumuni la: -

i. Kutoa maelekezo juu ya upatikanaji wa pembejeo za ruzuku na mabomba katika zao la korosho msimu wa 2022/2023;
ii. Kutoa maelekezo kuhusu utaratibu wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima msimu wa 2022/2023; na
iii. Kuainisha majukumu ya kila mdau katika usimamizi wa zoezi zima la usambazaji na ugawaji wa pembejeo za ruzuku.

## 4.0 MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA UTAYARISHAJI WA MWONGOZO HUU

Mbinu mseto zimefanikisha maandalizi ya Mwongozo huu ikiwa ni pamoja na mapitio ya Mwongozo uliotumika msimu wa 2021/2022. Aidha, mbinu shirikishi *(Participatory approach)* imetumika katika utayarishaji wa Mwongozo huu kwa kushirikisha makundi yote ya wadau katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho hapa nchini zikiwemo Mamlaka za Serikali ngazi ya Mikoa, ngazi ya Wilaya, Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali. Mathalani, kikao kazi cha kupitia rasimu ya kwanza kilihusisha wataalam wa kilimo kutoka Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri, Taasisi za Utafiti wa Kilimo, TPHPA, Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) na CBT. Hivyo, ni matumaini ya Serikali kuwa utekelezaji wa Mwongozo huu utakuwa shirikishi na utaleta manufaa yaliyokusudiwa kwa wadau wote katika Tasnia ya Korosho hapa nchini.

## 5.0 UPATIKANAJI WA PEMBEJEO NA MABOMBA KATIKA ZA ZAO LA KOROSHO MSIMU WA MWAKA 2022/2023

Kamati ya Pamoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika ambavyo ni MAMCU Ltd na TANECU Ltd kutoka Mkoa wa Mtwara, RUNALI na LMCU kutoka Mkoa wa Lindi, TAMCU Ltd kutoka Mkoa wa Ruvuma na CORECU Ltd kutoka Mkoa wa Pwani chini ya usimamizi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Naliendele na TPHPA ilianza mchakato wa kupata

wazabuni wa kuagiza na kusambaza viuatilifu (Sulphur tani 25,000; na viuatilifu vya maji lita 1,500,000), mabomba 3,500 na magunia 4,400,000 tangu mwezi Agosti, 2021. Jumla ya wazabuni kumi (10) kati ya hao wazabuni sita wa viuatilifu tu, mzabuni mmoja wa pembejeo na mabomba, na wazabuni watatu wa magunia walipatikana na kufunga mikataba mwishoni mwa mwezi Novemba, 2021. Sheria ya Manunuzi ya Umma kupitia zabuni shindani ya kitaifa *(National Competitive Tendering - NCT)* ndiyo iliyotumika kuwapata wazabuni hao. Kwa mujibu wa mikataba hiyo viuatilifu vyote vinatakiwa viwe vimesambazwa kwa Kamati ya Pamoja kupitia ghala kuu zilizopo Mtwara Mjini ifikapo mwisho wa mwezi Aprili, 2022 na mabomba mwisho wa mwezi Mei, 2022. **Jedwali Na. 2** linaonesha wazabuni na kiasi cha bidhaa wanazotakiwa kusambaza kwa mujibu wa mikataba.

**Jedwali Na. 2: Wazabuni na kiasi cha viuatilifu na mabomba wanayotakiwa kusambaza kwa mujibu wa mikataba.**

| Na. | Aina ya Bidhaa | Wazabuni | Jina la Biashara | Kipimo | Kiasi kwa Mujibu wa Mkataba |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Sulphur ya unga kwa ajili ya kuzuia ugonjwa wa ubwiriunga. | Suba Agro | Sulphur Dangoti | Tani | 8,000 |
| | | Bens Agrostar | Bens Sulphur | Tani | 10,000 |
| | | Prosperity | Makonde Sulphur | Tani | 1,000 |
| | | Faham Africa | Faru Sulphur | Tani | 1,000 |
| | | JM Traders | Kings Sulphur | Tani | 5,000 |
| | | **Jumla Sulphur ya Unga** | | | **25,000** |
| 2 | Viuatilifu vya sumu kudhibiti mbu wa mikorosho. | Bambana | Balacy 5 EC | Lita | 100,000 |
| | | Mo Green | Mo Karatep | Lita | 100,000 |
| | | Suba Agro | Subachlor | Lita | 100,000 |
| | | **Jumla Ndogo** | | | **300,000** |
| 3 | Viuatilifu vya sumu kudhibiti vidung'ata wa mikorosho. | Bambana | Balacy Super | Lita | 50,000 |
| | | Mo Green | Mocron | Lita | 50,000 |
| | | **Jumla Ndogo** | | | **100,000** |
| 4 | Viuatilifu vya Maji kudhibiti ubwiriunga na blaiti *(Duo purpose)*. | Bens Agrostar | Indazole | Lita | 540,000 |
| | | Suba Agro | Subatex | Lita | 360,000 |
| | | **Jumla Ndogo** | | | **900,000** |
| 5 | Viuatilifu vya maji kudhibiti ubwiriunga *(Single purpose)*. | Mo Green | Movil | Lita | 200,000 |
| | | **Jumla Ndogo** | | | **200,000** |
| | | **Jumla Viuatilifu vya Maji** | | | **1,500,000** |
| 6 | Mabomba | Faham Africa | Shogun | Idadi | 3,500 |
| | | **Jumla Mabomba *(Motorised blowers)*** | | | **3,500** |

**Chanzo:** Kamati ya Pamoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika.

## 6.0 UDHIBITI WA UBORA WA PEMBEJEO NA MABOMBA

Ili kudhibiti ubora wa bidhaa ikiwa ni pamoja na kujiridhisha na kiasi/ujazo kabla ya kusambazwa kwa wakulima; Kamati ya Pamoja imeandaa ghala kuu zilizopo Mtwara Mjini eneo la Bandari ya Mtwara. Ghala hizo ambazo zipo chini ya uangalizi wa Meneja Dhamana Kampuni ya ACE Global zitapokea, kuhifadhi na kusimamia utoaji wa pembejeo na kwa upande wa Kamati ya itakuwa na jukumu la kujiridhisha na ubora na kiasi cha bidhaa husika kilicholetwa na mzabuni kabla ya kusambazwa kwa wakulima. Sampuli itachukuliwa na kupelekwa TPHPA kwa ajili ya vipimo kwa kila toleo *(Batch No.)* la bidhaa husika. Viuatilifu vitakavyobainika kuwa na ubora unaostahili ndio vitasambazwa kwa wakulima. Bidhaa zote zitakazokuwa chini ya kiwango hazitaruhusiwa kusambazwa kwa wakulima.

## 7.0 MGAO WA PEMBEJEO NA MABOMBA

Kigezo kilichotumika kuagiza pembejeo na mabomba kama ilivyotajwa hapo juu ni uwezo wa kifedha *(Financial Capability)*. Aidha, ilibainika kwamba ili kutosheleza mahitaji ya pembejeo na mabomba katika zao la korosho hapa nchini zinahitajika zaidi ya tani 45,000 za sulphur ya unga, zaidi ya lita 2,500,000 za viuatilifu vya maji na zaidi ya mabomba 10,000. Hivyo, ni dhahiri kwamba kiasi cha pembejeo na mabomba yatakayosambazwa kwa wakulima msimu wa 2022/2023 hayatatosheleza mahitaji yao halisi.

Kufuatia hali hiyo kigezo cha uzalishaji wa korosho ghafi msimu wa mwaka 2021/2022 kimetumika kupata mgao wa pembejeo na mabomba ngazi ya Mikoa na Halmashauri zinazohusika na kilimo cha korosho hapa nchini. Aidha, kwa upande wa mikoa mipya kigezo cha idadi ya mikorosho kimeshauriwa kutumika badala ya uzalishaji kwani mikorosho yao mingi ni midogo. ***Kiambatisho Na, 1*** kinaonesha mgao wa pembejeo na mabomba kwa Mikoa na Halmashauri Msimu wa Mwaka 2022/2023. Hivyo, pamoja na ruzuku hii endapo itatokea mgao wa pembejeo aliopatiwa mkulima kutototosheleza mahitaji yake halisi, anashauriwa kujipatia kiasi kilichopungua sokoni (kutoka kwa wasambazaji na wauzaji waliothibitishwa na TPHPA).

## 8.0 UTARATIBU WA UGAWAJI WA PEMBEJEO NA MABOMBA KWA WAKULIMA

Kamati ya Pembejeo ya Mkoa itapokea mgao wa pembejeo na mabomba kutoka kwa Kamati ya Mapokezi na Usambazaji wa Pembejeo itakayoongozwa na TPHPA. Katika ngazi ya Wilaya, Kamati ya Pembejeo ya Wilaya ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya itapokea mgao kutoka kwa Kamati ya Pembejeo ya Mkoa. Kamati ya Pembejeo ya Wilaya itagawa pembejeo na mabomba kwenye kata na vijiji kwa kuzingatia takwimu za uzalishaji wa korosho ghafi za msimu uliopita. Kamati ya Pembejeo ya Kata itawasilisha mgao wa pembejeo na mabomba kwa Kamati ya Pembejeo ya Kijiji kwa ajili ya ugawaji kwa wakulima kwa kuzingatia idadi ya mikorosho na uzalishaji wa korosho ghafi za msimu uliopita.

Vigezo vitakavyotumika na Kamati ya Pembejeo ya Kijiji kugawa pembejeo kwa wakulima ni:-

(i) Awe mkulima wa korosho;
(ii) Awe amesafisha shamba lake la korosho;
(iii) Awe anajua idadi kamili ya mikorosho na kiasi cha korosho ghafi alizovuna msimu uliopita;
(iv) Shamba lake liwe ndani ya eneo la kijiji husika;
(v) Awe amekubalika pasi na shaka mbele ya mkutano wa kijiji kuwa yeye ni mkulima wa korosho ndani ya kijiji hicho;

(vi) Awe tayari kutumia elimu ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kama itakavyotolewa na Afisa Ugani wa Kijiji au Kata; na

(vii) Vigezo vingine kama vitakavyowekwa na Kamati ya Pembejeo ya Wilaya kwa lengo la kuongeza ufanisi wa ugawaji wa pembejeo kwa wakulima.

Hatua zinazopaswa kufuatwa na mkulima ili aweze kupata pembejeo bila malipo, kwanza kujiandikisha kwenye daftari la ugawaji wa pembejeo za zao la korosho lililopo kwa Mtendaji wa Kijiji husika. Pili, kuhudhuria mkutano wa kijiji utakaohakiki majina ya wakulima wa korosho na mgao wao wa pembejeo. Na tatu, kuheshimu matokeo ya uhakiki wa majina ya wakulima wa korosho waliopitishwa na mkutano wa kijiji kupata pembejeo za zao la korosho msimu wa 2022/2023.

Kamati ya Pembejeo ya Kijiji itatakiwa kuhakikisha kwamba orodha ya wakulima waliopitishwa na mkutano wa kijiji kupata pembejeo za zao la korosho kwa kuzingatia vigezo tajwa hapo juu inabandikwa kwenye mbao za matangazo za ofisi ya Kijiji. Lengo la hatua hii ni kupanua wigo wa uwazi *(Transparency)* na kutoa nafasi kwa wakulima kujiridhisha na uhalisia wa mgao uliotolewa kwa kuzingatia vigezo vilivyotajwa hapo juu.

Aidha, endapo mkulima atakuwa na malalamiko, Mtendaji wa Kata husika atatakiwa kuyapokea na kuyawasilisha kwa Kamati ya Pembejeo ya Kata kwa ajili ya utatuzi. Na endapo itashindikana au mkulima hatoridhika na uamuzi kutoka Kamati ya Pembejeo ya Kata anaruhusiwa kukata rufaa kwa kupeleka shauri lake kwa Kamati ya Pembejeo ya Wilaya kupitia kwa Katibu Tawala wa Wilaya *(DAS)* husika. Maamuzi ya Kamati ya Pembejeo ya Wilaya yatakuwa ya mwisho na taarifa itawasilishwa kwa Kamati ya Pembejeo ya Mkoa husika na Bodi ya Korosho Tanzania kwa ajili ya kumbukumbu.

Wakulima waliokuwa wamechangia pembejeo kabla ya Serikali kusitisha uchangiaji; Sambamba na kurejeshewa fedha walizochangia watatakiwa kupewa kipaumbele katika mgao wa pembejeo kutegemea na hali ya upatikanaji wa pembejeo na mabomba katika eneo husika. Aidha, Fedha walizorejeshewa zitumike kwenye shughuli za maandalizi ya shamba la mikorosho kama vile ununuzi wa pembejeo sokoni ili kutosheleza mahitaji, palizi, upuliziaji na shughuli zingine za shamba.

Wakati wa kuchukua pembejeo kutoka kwenye Kamati ya Pembejeo ya Kijiji mkulima atatakiwa kusaini stakabadhi ya kukiri kuchukua pembejeo/mabomba ambayo pamoja na mambo mengine itaonesha jina kamili la mkulima, namba yake ya simu, kijiji/mtaa anaoishi, jina la viuatilifu alivyochukua, kiasi na thamani yake. Mgawanyo wa nakala ya stakabadhi hiyo ni kama ifuatavyo:

(i) Nakala Halisi - Mkulima;
(ii) Nakala ya Kwanza - Halmashauri ya Wilaya/Mji;
(iii) Nakala ya Pili - Mtendaji wa Kijiji;
(iv) Nakala ya Tatu - Bodi ya Korosho Tanzania; na
(v) Nakala ya Nne (Kitabuni) - Kamati ya Pamoja ya Vyama vya Ushirika.

***MUHIMU:*** Kamati ya Pamoja ihakikishe inaandaa nakala za kutosha za vitabu hivi na kusambaza kwa wakati kwenye Kamati za Pembejeo za Vijiji. Vitabu hivyo ndivyo vitakavyotumiwa na Kamati ya Pembejeo ya Kijiji kugawa pembejeo na mabomba kwa wakulima.

## 9.0 MUUNDO WA KAMATI YA MAPOKEZI, KAMATI ZA PEMBEJEO WILAYA, KATA NA KIJIJI

Muundo wa Kamati zilizotajwa hapo juu ni kama ifuatavyo: -

### 9.1 Kamati ya Mapokezi na Usambazaji wa Pembejeo na Mabomba

(i) Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) - Mwenyekiti
(ii) Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara - Mjumbe
(iii) Ofisi ya Usalama wa Taifa - Mjumbe
(iv) Bodi ya Korosho Tanzania – Katibu
(v) TARI Naliendele - Mjumbe
(vi) Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania - Mjumbe
(vii) Chama Kikuu cha Ushirika MAMCU Ltd - Mjumbe

### 9.2 Kamati ya Pembejeo ya Mkoa

(i) Mkuu wa Mkoa – Mwenyekiti
(ii) Katibu Tawala wa Mkoa – Katibu
(iii) Wawakilishi wawili kutoka Sekretarieti ya Mkoa - Mjumbe
(iv) Afisa Usalama wa Mkoa (RSO) - Mjumbe
(v) Vyama Vikuu vya Ushirika – Mjumbe

### 9.3 Kamati ya Pembejeo ya Wilaya

(i) Mkuu wa Wilaya - Mwenyekiti
(ii) Mkurugenzi wa Halmashauri - Katibu
(iii) Kamati ya Ulinzi na Usalama - Mjumbe
(iv) Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika – Mjumbe
(v) Mratibu wa Zao la Korosho *(DSMS – Cashew)* - Mjumbe

### 9.4 Kamati ya Pembejeo ya Kata

(i) Mtendaji wa Kata - Mwenyekiti

(ii) Watendaji wa Vijiji vya Kata husika – Mjumbe (Mtendaji wa Kijiji Mwenyeji atakuwa Katibu)
(iii) Afisa Kilimo wa Kata – Mjumbe
(iv) Mwenyekiti na Katibu wa AMCOS husika - Mjumbe

### 9.5 Kamati ya Pembejeo ya Kijiji

(i) Mtendaji wa Kijiji - Mwenyekiti
(ii) Afisa Kilimo wa Kijiji – Katibu
(iii) Wakulima Viongozi wa Korosho Watatu wa Kijiji husika - Mjumbe

***MUHIMU:*** Wakulima Viongozi wa Korosho wachaguliwe na wananchi kwenye Mkutano mmojawapo wa Kijiji.

## 10.0 UTARATIBU WA USAFIRISHAJI WA PEMBEJEO NA MABOMBA KUTOKA GHALA KUU KWENDA KWA WAKULIMA

Usafirishaji wa pembejeo na mabomba kutoka maghalani Mtwara kwenda vijijini utafanywa na Chama Kikuu cha Ushirika husika. Katika kijiji pembejeo na mabomba yatapokelewa na Kamati ya Pembejeo ya Kijiji kwenye ghala la Chama cha Msingi au ghala la kijiji kadri kamati hiyo itakavyoona inafaa. Kiasi cha pembejeo na mabomba kitakachokuwa kikisafirishwa kitazingatia mchanganuo wa usafirishaji wa pembejeo kama utakavyokuwa umeandaliwa na Kamati ya Mapokezi na Usambazaji wa Pembejeo na Mabomba. Aidha, ni jukumu la Vikosi Kazi vya Mikoa na Wilaya husika kufuatilia na kuhakikisha kuwa pembejeo na mabomba vinafika kwa wakulima vikiwa katika kiasi na kiwango kile kile kama kilivyotoka kwenye maghala yaliyopo Mtwara Mjini.

## 11.0 USIMAMIZI, UFUATILIAJI NA TATHMINI

Kila Mkoa utatakiwa kuwa na Kikosi Kazi cha Mkoa kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia zoezi la usambazaji wa viuatilifu vya ruzuku na mabomba ndani ya Mkoa. Kikosi kazi hicho kitahusisha wajumbe kutoka Sekretarieti ya Mkoa, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Vyama Vikuu vya Ushirika. Aidha, kutakuwa na vikao vya tathmini vitakavyokuwa vikifanyika mara moja kwa mwezi kipindi cha chote cha usambazaji na ugawaji wa pembejeo ili kufanya uchambuzi wa kina wa changamoto na kuchukua hatua kwa wakati.

## 12.0 UTARATIBU WA UGHARAMIAJI KWA WANAOHUSIKA NA USIMAMIZI

Kwa kuwa wahusika katika shughuli ya usambazaji wa viuatilifu na mabomba kwa namna moja ama nyingine ni wanufaika *(Beneficiaries)* wa zao la korosho hapa nchini; kila kamati itatakiwa kujigharamia ili kuweza kufikia malengo ya uzalishaji wa korosho ghafi tani 400,000 msimu wa 2022/2023 na tani 700,000 ifikapo msimu wa mwaka 2025/2026.

## 13.0 MAFUNZO YA MATUMIZI SAHIHI NA SALAMA YA VIUATILIFU NA MABOMBA

Jukumu la kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu na mabomba ni la wahusika wote ikiwa ni pamoja na Sekretarieti ya Mkoa, Halmashauri, Wazabuni wa Viuatilifu na Mabomba, Bodi ya Korosho Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania, TARI Naliendele na Vyama Vikuu vya Ushirika. Aidha, kila mzabuni aliyesambaza viuatilifu na/au mabomba atatakiwa kuchangia gharama za kuendesha mafunzo hayo kupitia utaratibu maalum utakaotolewa na Bodi ya Korosho Tanzania. Mafunzo yatatolewa kwa maafisa ugani kilimo wote waliopo kwenye maeneo yanayozalisha korosho, wapuliziaji na wakulima viongozi ambao watawajibika kufundisha wakulima wengine katika maeneo yao.

## 14.0 UGHARAMIAJI WA PEMBEJEO NA MABOMBA

Kwa upande wa viuatilifu vya ruzuku mkulima hatachangia chochote. Hii ni utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Serikali kupitia kwa Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein M. Bashe (Mb.) tarehe 08 Aprili, 2022 Jijini Dodoma. Aidha, kwa upande wa mabomba ya kupulizia mkulima atatakiwa kuchangia nusu ya gharama kupitia akaunti itakayoelekezwa na Chama Kikuu cha Ushirika husika.

## 15.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU

Ili kuhakikisha zoezi la ugawaji wa pembejeo na mabomba katika zao la korosho msimu wa 2022/2023 unafanikiwa, majukumu ya kiutendaji na kitaasisi yamegawanywa kama ilivyoelezwa hapo chini: -

### 15.1 Wizara ya Kilimo

(i) Kutoa na kusimamia miongozo ya kisera juu ya ununuzi na usambazaji wa pembejeo na vifungashio vya mazao ya wakulima;

(ii) Kuunganisha Tasnia ya Korosho na Sekta zingine za uchumi ikiwa ni pamoja na Wizara nyingine nchini; na

(iii) Kusimamia upatikanaji wa pembejeo na mabomba kwa wakulima.

### 15.2 Sekretarieti za Mikoa

(i) Kuratibu makadirio ya mahitaji ya pembejeo na mabomba katika ngazi ya Mkoa;

(ii) Kuratibu mgawo wa pembejeo na mabomba kwenda katika kamati za pembejeo na wakulima kwa kuzingatia kigezo cha uzalishaji;

(iii) Kusimamia na kufuatilia zoezi zima la usambazaji wa pembejeo na mabomba;

(iv) Kuratibu upatikanaji, usambazaji na utunzaji wa taarifa za usambazaji wa pembejeo na mabomba; na

(v) Kuchukua hatua za kisheria kwa mtu yeyote atakayebainika kukiuka

utaratibu wa usambazaji na ugawaji wa pembejeo na mabomba kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika; na

(vi) Kuhakikisha uwepo wa Kamati za pembejeo za Wilaya; Kata na Vijiji.

### 15.3 Bodi ya Korosho Tanzania

(i) Kusimamia masuala yote ya kisheria yanayohusu upokeaji, usambazaji wa pembejeo na mabomba yanayosambazwa kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika;

(ii) Kuunda na kuratibu utendaji wa Kamati ya Mapokezi ya Pembejeo na Mabomba;

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya pembejeo, mabomba na magunia iliyofungwa kati ya wazabuni na Kamati ya Pamoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika;

(iv) Kuhakikisha pembejeo na mabomba yanawafikia wakulima kwa wakati, kiasi na ubora kama ilivyopangwa;

(v) Kutoa Mwongozo wa ugawaji wa pembejeo na mabomba yanayosambazwa kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika;

(vi) Kufuatilia, kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza taarifa zinazohusu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za zao la korosho na mabomba hapa nchini; na

(vii) Kuratibu mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu na mabomba.

### 15.4 Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)

(i) Kutoa waraka unaoainisha wajibu wa Vyama vya Ushirika husika katika kutekeleza maelekezo ya Serikali juu ya uagizaji na usambazaji wa pembejeo na mabomba kwa ajili ya msimu wa 2022/2023;

(ii) Kusimamia zoezi la utangazaji wa zabuni ya pamoja ya pembejeo na mabomba;

(iii) Kusimamia usambazaji na ugawaji wa pembejeo na mabomba;

(iv) Kuhakikisha pembejeo na mabomba yanawafikia wakulima kwa wakati, kiasi na ubora kama ilivyopangwa.

(v) Kufuatilia ukusanyaji wa fedha za mabomba; na

(vi) Kusimamia ulipaji wa fedha kwa wazabuni.

### 15.5 Halmashauri

(i) Kukusanya taarifa za makadirio ya mahitaji ya pembejeo na mabomba katika msimu husika;

(ii) Kuhakikisha taarifa ya mgao wa pembejeo na mabomba zinabandikwa kwenye mbao za matangazo za Halmashauri, Kata, Vijiji na AMCOS;

(iii) Kusimamia usambazaji na ugawaji wa pembejeo na mabomba na kuhakikisha kuwa zinawafikiwa wakulima kwa wakati;
(iv) Kupanga ratiba ya upuliziaji wa viuatilifu na kufuatilia ufanisi wa viuatilifu hivyo baada ya kupulizwa;
(v) Kusimamia na kufuatilia uchukuaji wa pembejeo na mabomba kutoka maghalani Mtwara kwenda vijijini;
(vi) Kuhakikisha kuwa kila mkulima aliyeorodheshwa kupata pembejeo anapata kulingana na mgao na kiasi halisi kilichosambazwa;
(vii) Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo ndani ya Halmashauri husika;
(viii) Kuhakiki taarifa za ugawaji wa pembejeo na mabomba kwa wakulima na kuthibitisha usahihi wake; na
(ix) Kuchukua hatua za kisheria kwa mtu yeyote atakayebainika kukiuka taratibu za ugawaji wa pembejeo ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwenye mamlaka husika.

### 15.6 Vyama Vikuu vya Ushirika *(Union)*

(i) Kufanya manunuzi ya pamoja ya pembejeo na mabomba kwa kuzingatia taratibu, miongozo, kanuni na sheria zilizopo;
(ii) Kuandaa nyaraka za mapokezi na ugawaji wa pembejeo na mabomba;
(iii) Kuandaa maghala ya kupokelea pembejeo na mabomba kutoka kwa wazabuni;
(iv) Kupokea pembejeo na mabomba kutoka kwa wazabuni;
(v) Kugharamia usafirishaji wa pembejeo na mabomba kwenda Halmashauri husika hadi ngazi ya Kijiji;
(vi) Kusimamia na kufuatilia usambazaji na ugawaji wa pembejeo na mabomba;
(vii) Kutunza kumbukumbu zote za uagizaji, usambazaji na ugawaji wa pembejeo na mabomba;
(viii) Kupitia na kuhakiki nyaraka/ankara za madai kwa lengo la kujiridhisha kwamba ziko sahihi kabla ya kuwalipa wazabuni; na
(ix) Kulipa wazabuni kwa kuzingatia mkataba.

### 15.7 Chama cha Msingi cha Ushirika (AMCOS)

(i) Kutoa ushirikiano kwa Serikali ya Kijiji/Vijiji katika kuhakiki orodha ya wakulima wa zao la korosho kwa ajili ya kupata pembejeo.

### 15.8 TARI Naliendele

(i) Kuthibitisha matumizi ya pembejeo husika kwenye zao la korosho;
(ii) Kufuatilia mwenendo wa uzalishaji na hali ya hewa na kutoa ushauri wa matumizi ya viuatilifu;
(iii) Kutoa mapendekezo ya pembejeo zinazofaa kuagizwa na kusambazwa kwa wakulima nchini; na

(iv) Kutoa ushauri wa kitaalam kwenye Kamati ya Ununuzi wa Pamoja wa pembejeo na mabomba.

### 15.9 Mamlaka ya Udhibiti wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA)

(i) Kuainisha viambata amilifu (*Active ingredients*) kwenye viuatilifu vya zao la korosho kwa lengo la kulinda viwango na ubora;
(ii) Kutoa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa Maafisa Kilimo, Wauzaji wa Pembejeo, Wapuliziaji na Wakulima; na
(iii) Kufanya ukaguzi mara kwa mara wa viuatilifu vya korosho vinavyotumika nchini.

### 15.10 Kamati ya Mapokezi na Ugawaji wa Pembejeo

(i) Kujiridhisha na ubora wa kiuatilifu kabla ya kupokelewa;
(ii) Kupokea na kuhifadhi viuatilifu vinavyoletwa na wazabuni;
(iii) Kugawa viuatilifu kwenda Halmashauri kwa kuzingatia mchanganuo wa mgao uliowasilishwa; na
(iv) Kuratibu masuala yote ya mapokezi na ugawaji wa pembejeo na mabomba.

### 15.11 Kamati ya Pembejeo ya Wilaya

(i) Kuratibu makadirio ya mahitaji ya pembejeo za zao la korosho;
(ii) Kuunda kamati za pembejeo za Wilaya, Kata na Vijiji ambazo zitasimamia na kufuatilia kwa karibu zoezi la ugawaji wa pembejeo kwa wakulima;
(iii) Kusimamia na kufuatilia zoezi zima la ugawaji wa pembejeo na mabomba kwa wakulima;
(iv) Kuchukua hatua za kisheria kwa mtu yeyote atakayebainika kukiuka taratibu za ugawaji wa pembejeo; na
(v) Kuunda kikosi kazi kitakachosimamia usambazaji na ugawaji wa pembejeo na mabomba kwa wakulima ndani ya Wilaya.

### 15.12 Kamati ya Pembejeo ya Mkoa

(i) Kufanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye ngazi ya Halmashauri, Kata na Vijiji kujiridhisha na kiwango cha uzingatiaji wa utaratibu wa ugawaji wa pembejeo na mabomba kwa mujibu wa Mwongozo huu; na
(ii) Kuhakikisha kuwa yeyote atakayekutwa akichepusha pembejeo na mabomba anachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo.

### 15.13 Wazabuni wa Pembejeo na Mabomba

(i) Kusambaza pembejeo na mabomba kwa Vyama Vikuu vya Ushirika kwa mujibu wa mkataba;

(ii) Kuhakikisha kuwa amesajiliwa au anatambulika na Serikali ya Kijiji kuwa yeye ni mkulima wa korosho;
(iii) Kuhakikisha kuwa shamba lake ni safi;
(iv) Kusaini fomu ya kukiri kuchukua pembejeo wakati wa kukabidhiwa pembejeo mbele ya Kamati ya Pembejeo ya Kijiji husika;
(v) Kutumia pembejeo kwa usahihi, yaani kutimiza idadi ya mipulizo inayotakiwa na kutumia viwango na vipimo sahihi kama inavyoelekezwa na mtaalam wa kilimo (Afisa Kilimo) aliyepo katika eneo lake;
(vi) Kutunza kumbukumbu za matumizi ya pembejeo kwa kuandika kwenye daftari na kutunza nyaraka za uchukuaji wa viuatilifu na mabomba kutoka kwenye Kamati ya Pembejeo ya Kijiji; na
(vii) Kutoa taarifa kwa Kamati ya Pembejeo ya Kata juu ya ukiukwaji wowote wa Mwongozo huu.

### 15.17 Taasisi za Fedha

(i) Kutoa huduma za kifedha kwa wadau wa korosho nchini ikiwa ni pamoja na wakulima na wasambazaji wa pembejeo na mabomba; na
(ii) Kuchangia gharama za kuendesha mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu vya zao la korosho kwa wakulima.

### 15.18 Waandishi wa habari

(i) Kuhabarisha umma juu ya taarifa za upatikanaji, usambazaji, ugawaji na matumizi ya pembejeo na mabomba.

## 16.0 WAJIBU WA PAMOJA

(ii) Kuhakikisha majukumu haya yanatekelezwa kwa kuzingatia sera na sheria za nchi;
(iii) Kutoa taarifa mapema kuhusu suala lolote ambalo litakwamisha utekelezaji wa mpango huu;
(iv) Kuhakikisha pembejeo zinamnufaisha mkulima kama mtumiaji wa mwisho na sio mtu mwingine; na
(v) Kuhakikisha kila mdau husika anatimiza wajibu wake.

## 17.0 MUDA WA UTEKELEZAJI

Utekelezaji wa Mwongozo huu utakuwa kuanzia tarehe ya kutolewa kwa Mwongozo huu hadi kipindi chote cha msimu wa mwaka 2022/2023.

## 18.0 ILANI

Serikali haitawajibika kwa namna yoyote ile kwa mdau ambaye hatazingatia utaratibu uliowekwa kwenye Mwongozo huu.

## KIAMBATISHO NA. 1: MGAO WA PEMBEJEO NA MABOMBA YA RUZUKU KATIKA ZAO LA KOROSHO MSIMU WA MWAKA 2022/2023

| NA | MKOA | HALMASHAURI | UZALISHAJI WA KOROSHO GHAFI MSIMU WA 2021/2022 (KG) | ASILIMIA YA UZALISHAJI (%) | MGAO | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | SULPHUR YA UNGA (KG) | VIUATILIFU VYA SUMU VYA KUDHIBITI MBU WA MIKOROSHO (L) | VIUATILIFU VYA SUMU VYA KUDHIBITI VIDUNG'ATA WA MIKOROSHO (L) | VIUATILIFU VYA KUDHIBITI UBWIRIUNGA NA BLAITI *(DUAL PURPOSE)* (L) | VIUATILIFU VYA KUDHIBITI UBWIRIUNGA *(SINGLE PURPOSE)* (L) | MABOMBA (IDADI) |
| Kiasi cha pembejeo na mabomba kwa mujibu wa mikataba | | | | | 25,000,000 | 300,000 | 100,000 | 900,000 | 200,000 | 3,500 |
| 1 | Mtwara | Mtwara MC | 1,615,336 | 0.68 | 169,575 | 1,994 | 665 | 5,983 | 1,329 | 23 |
| | | Mtwara DC | 8,259,569 | 3.47 | 867,075 | 10,197 | 3,399 | 30,590 | 6,798 | 119 |
| | | Nanyamba TC | 13,497,958 | 5.67 | 1,416,992 | 16,664 | 5,555 | 49,991 | 11,109 | 194 |
| | | Tandahimba | 35,909,421 | 15.08 | 3,769,709 | 44,332 | 14,777 | 132,995 | 29,555 | 517 |
| | | Newala DC | 13,979,312 | 5.87 | 1,467,524 | 17,258 | 5,753 | 51,774 | 11,505 | 201 |
| | | Newala TC | 10,628,323 | 4.46 | 1,115,743 | 13,121 | 4,374 | 39,363 | 8,747 | 153 |
| | | Masasi DC | 24,598,308 | 10.33 | 2,582,288 | 30,368 | 10,123 | 91,103 | 20,245 | 354 |
| | | Masasi MC | 6,369,985 | 2.67 | 668,710 | 7,864 | 2,621 | 23,592 | 5,243 | 92 |
| | | Nanyumbu | 15,438,705 | 6.48 | 1,620,729 | 19,060 | 6,353 | 57,179 | 12,707 | 222 |
| | | **Jumla Ndogo** | **130,296,917** | **54.71** | **13,678,347** | **160,857** | **53,619** | **482,572** | **107,238** | **1,877** |
| 2 | Lindi | Lindi(MC) | 2,784,712 | 1.17 | 292,334 | 3,438 | 1,146 | 10,314 | 2,292 | 40 |
| | | Mtama | 9,344,120 | 3.92 | 980,930 | 11,536 | 3,845 | 34,607 | 7,690 | 135 |
| | | Nachingwea | 17,787,954 | 7.47 | 1,867,349 | 21,960 | 7,320 | 65,880 | 14,640 | 256 |
| | | Ruangwa | 13,123,948 | 5.51 | 1,377,730 | 16,202 | 5,401 | 48,606 | 10,801 | 189 |
| | | Liwale | 15,481,950 | 6.50 | 1,625,269 | 19,113 | 6,371 | 57,339 | 12,742 | 223 |
| | | Kilwa | 7,484,510 | 3.14 | 785,711 | 9,240 | 3,080 | 27,720 | 6,160 | 108 |
| | | **Jumla Ndogo** | **66,007,194** | **27.72** | **6,929,322** | **81,489** | **27,163** | **244,466** | **54,326** | **951** |
| 3 | Pwani | Mkuranga | 4,330,527 | 1.82 | 454,611 | 5,346 | 1,782 | 16,039 | 3,564 | 62 |
| | | Kibaha TC | 204,700 | 0.09 | 21,489 | 253 | 84 | 758 | 168 | 3 |
| | | Kibaha DC | 523,460 | 0.22 | 54,952 | 646 | 215 | 1,939 | 431 | 8 |
| | | Bagamoyo | 113,305 | 0.05 | 11,895 | 140 | 47 | 420 | 93 | 2 |
| | | Rufiji | 2,901,764 | 1.22 | 304,622 | 3,582 | 1,194 | 10,747 | 2,388 | 42 |
| | | Kisarawe | 50,200 | 0.02 | 5,270 | 62 | 21 | 186 | 41 | 1 |
| | | Mafia | 76,670 | 0.03 | 8,049 | 95 | 32 | 284 | 63 | 1 |
| | | Kibiti | 7,623,439 | 3.20 | 800,296 | 9,411 | 3,137 | 28,234 | 6,274 | 110 |
| | | Chalinze | 38,000 | 0.02 | 3,989 | 47 | 16 | 141 | 31 | 1 |
| | | **Jumla Ndogo** | **15,862,065** | **6.66** | **1,665,172** | **19,582** | **6,527** | **58,747** | **13,055** | **228** |
| 4 | Ruvuma | Tunduru | 24,617,262 | 10.34 | 2,584,278 | 30,391 | 10,130 | 91,173 | 20,261 | 355 |
| | | Songea | 10,774 | 0.005 | 1,131 | 13 | 4 | 40 | 9 | 0 |
| | | Mbinga | 33,876 | 0.01 | 3,556 | 42 | 14 | 125 | 28 | 0 |
| | | Namtumbo | 566,235 | 0.24 | 59,442 | 699 | 233 | 2,097 | 466 | 8 |
| | | Nyasa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| | | Madaba | 14,377 | 0.01 | 1,509 | 18 | 6 | 53 | 12 | 0 |
| | | **Jumla Ndogo** | **25,242,524** | **10.60** | **2,649,917** | **31,163** | **10,388** | **93,489** | **20,775** | **364** |
| 5 | Tanga | Muheza | 24,450 | 0.01 | 2,567 | 30 | 10 | 91 | 20 | 0 |
| | | Pangani | 75,439 | 0.03 | 7,919 | 93 | 31 | 279 | 62 | 1 |
| | | Tanga | 63,077 | 0.03 | 6,622 | 78 | 26 | 234 | 52 | 1 |
| | | Korogwe TC | 26,486 | 0.01 | 2,780 | 33 | 11 | 98 | 22 | 0 |
| | | Korogwe DC | 85,578 | 0.04 | 8,984 | 106 | 35 | 317 | 70 | 1 |
| | | Mkinga | 454,943 | 0.19 | 47,759 | 562 | 187 | 1,685 | 374 | 7 |
| | | Handeni | 5,814 | 0.00 | 610 | 7 | 2 | 22 | 5 | 0 |
| | | **Jumla Ndogo** | **735,787** | **0.31** | **77,242** | **908** | **303** | **2,725** | **606** | **11** |
| | **Jumla Mikoa ya Asili** | | **238,144,487** | **100** | **25,000,000** | **294,000** | **98,000** | **882,000** | **196,000** | **3,430** |
| 6 | Tengo la 2% ya Viuatilifu vya Maji kwa ajili ya Mikoa mipya. | | | | | 6,000 | 2,000 | 18,000 | 4,000 | 70 |
| | **Jumla Mikoa Mipya** | | | | - | **6,000** | **2,000** | **18,000** | **4,000** | **70** |
| **JUMLA KUU** | | | | | **25,000,000** | **300,000** | **100,000** | **900,000** | **200,000** | **3,500** |

***NB: Halmashauri zenye mgao sifuri wa mabomba zitatengewa kutoka kwenye mikoa mipya.***

**Nyongeza Na. 01**

# WIZARA YA KILIMO

# BODI YA KOROSHO TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MABORESHO YA MWONGOZO WA UPATIKANAJI NA UGAWAJI WA PEMBEJEO BILA MALIPO KWA WAKULIMA NA MABOMBA YA RUZUKU KATIKA ZAO LA KOROSHO MSIMU WA 2022/2023 UNAOTOLEWA CHINI YA SHERIA YA TASNIA YA KOROSHO NA. 18 YA MWAKA 2009 NA KANUNI ZAKE ZA MWAKA 2010

### 1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Upokeaji na Usambazaji wa Viuatilifu kwa kushirikiana na wadau ikiwa ni pamoja na Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Vyama vya Ushirika imeanza ugawaji na usambazaji wa pembejeo za zao la korosho kwa wakulima msimu wa mwaka 2022/23 baada ya uzinduzi kufanyika Mjini Mtwara tarehe 17 Mei 2022.

Ili kuimarisha usimamizi na uratibu wa usambazaji wa pembejeo hizo kwa wakulima, mnamo tarehe 09 Mei, 2022; Bodi ilitoa ***"Mwongozo wa Upatikanaji na Ugawaji wa Pembejeo bila Malipo kwa Wakulima na Mabomba ya Ruzuku katika Zao la Korosho Msimu wa 2022/2023"***. Mwongozo huo, pamoja na mambo mengine uliainisha utaratibu wa ugawaji na usambazaji wa pembejeo na mabomba ya ruzuku msimu wa mwaka 2022/23.

Kufuatia maoni yaliyotolewa na wadau wa Tasnia ya Korosho, Bodi ya Korosho Tanzania imefanya maboresho kwenye usimamizi na uratibu wa ugawaji na usambazaji wa pembejeo msimu wa mwaka 2022 katika Ukurasa Na. 9 Kifungu 9.0 kinachohusu muundo wa Kamati za Pembejeo kuanzia kipengele Na. 9.3; hadi 9.5 kwa kuongeza Wajumbe wa Kamati kama inavyoonekana katika ukurasa Na. 2 hapa chini.

## 2.0 MABORESHO YA MUUNDO WA KAMATI ZA PEMBEJEO NGAZI YA WILAYA, KATA NA VIJIJI

| NA. | MUUNDO WA KAMATI WA AWALI | MUUNDO WA KAMATI BAADA YA MABORESHO |
|---|---|---|
| 9.3 | **Kamati ya Pembejeo ya Wilaya**<br>(i) Mkuu wa Wilaya - Mwenyekiti<br>(ii) Mkurugenzi wa Halmashauri - Katibu<br>(iii) Kamati ya Ulinzi na Usalama - Mjumbe<br>(iv) Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika – Mjumbe<br>(v) Mratibu wa Zao la Korosho *(DSMS – Cashew)* - Mjumbe | **Kamati ya Pembejeo ya Wilaya**<br>(i) Mkuu wa Wilaya – Mwenyekiti<br>(ii) Mkurugenzi wa Halmashauri – Katibu<br>(iii) Mwenyekiti wa Halmashauri/ Mstahiki Meya - Mjumbe<br>(iv) Kamati ya Ulinzi na Usalama - Mjumbe<br>(v) Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika – Mjumbe<br>**(vi)** Mratibu wa Zao la Korosho *(DSMS – Cashew)* – Mjumbe<br>(vii) Mwakilishi wa Chama Kikuu husika |
| 9.4 | **Kamati ya Pembejeo ya Kata**<br>(i) Afisa Mtendaji Kata - Mwenyekiti<br>(ii) Watendaji wa Vijiji wa Kata husika - Wajumbe (Mtendaji wa Kijiji Mwenyeji atakuwa Katibu)<br>(iii) Afisa Kilimo wa Kata - Mjumbe<br>(iv) Mwenyekiti na Katibu wa AMCOS | **Kamati ya Pembejeo ya Kata**<br>(i) Diwani wa Kata - Mwenyekiti<br>(ii) Afisa Mtendaji Kata - Katibu<br>(iii) Watendaji wa Vijiji wa Kata husika - Wajumbe<br>(iv) Afisa Kilimo wa Kata - Mjumbe<br>(v) Mwenyekiti na Katibu wa AMCOS |
| 9.5 | **Kamati ya Pembejeo ya Kijiji**<br>i.Mtendaji wa Kijiji- Mwenyekiti<br>ii.Afisa Kilimo wa Kijiji- Katibu<br>iii.Wakulima Viongozi wa Korosho watatu wa Kijiji husika - Mjumbe | **Kamati ya Pembejeo ya Kijiji**<br>**i.**Mwenyekiti wa Kijiji – Mwenyekiti<br>ii. Mtendaji wa Kijiji – Katibu<br>iii.Afisa Kilimo wa Kijiji – Mjumbe<br>iv. Wakulima Viongozi wa Korosho watatu wa Kijiji Husika - Mjumbe |

Maboresho haya yasomwe sambamba na *"Mwongozo wa Upatikanaji na Ugawaji wa Pembejeo bila Malipo kwa Wakulima na Mabomba ya Ruzuku katika Zao la Korosho Msimu wa Mwaka 2022/2023"* Uliotolewa tarehe 9 Mei, 2022.

Imetolewa na:-

Francis Alfred
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**17 Mei 2022**